*Wekeza na jenga maisha na SACCOS*

# LESA SACCOS LTD

## REG. No DSR 1299

# SERA YA UHAMASIHAJI WA UNUNUAJI WA AKIBA, HISA NA AMANA

WEKA AKIBA MARA KWA MARA, KOPA KWA BUSARA LIPA KWA WAKATI, WEKEZA KWA MAENDELEO YAKO.

**Toleo la I-2020**

UIDHINISHAJI WA SERA YA UHAMASISHAJI UWEKAJI AKIBA, HISA NA AMANA

| **Tarehe ya Kupitishwa na Kikao Cha Bodi** | | **Kikao Cha Bodi Tarehe 17 Julai 2020** |
|---|---|---|
| **Mpya** | ☐ | **Toleo la; I Mwaka 2020** |
| **Imehuishwa** | ☐ | |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Wanachama na;**

| S/N | Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EVA. J. BOSCO | Mwenyekiti wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 2 | GWAMAKA JAPHARI | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 3 | SEMALY KISAMO | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 4 | SHAFII MMILE | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 5 | NAOMI SERBANTEZ | Mjumbe wa Bodi | | |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Watendaji na:**

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| DEONATUS KIHEKA | Meneja | | |

**Kwa Matumizi ya Mrajis:**

Maoni ya Mrajis:

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| | | | |

*Muhuri*

SEHEMU YA KWANZA ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Historia ........ 1
1.2 Madhumuni ya kuwa na Sera hii ........ 1
SEHEMU YA PILI ........ 2
2.0 HISA ........ 2
2.1 Maana ya Hisa ........ 2
2.2 Kiingilio ........ 2
2.3 Aina za Hisa ........ 3
2.4 Hisa za Hiari ........ 3
2.5 Ulipaji wa Hisa ........ 4
2.6 Ukomo wa Hisa kwa Mwanachama ........ 4
2.7 Kupunguza Hisa ........ 4
2.8 Taratibu za kupitishwa kuwa Mwanachama ........ 4
2.9 Haki ya Kupatiwa Huduma ........ 5
2.10 Gawio ........ 5
2.11 Uhamishaji wa Hisa ........ 7
2.12 Hisa Kutumika Kama Dhamana ya Mkopo ........ 7
2.13 Cheti cha Hisa ........ 7
2.14 Hisa Kushirikiliwa kama Mali katika mchakato wa Ufilisi ........ 7
2.15 Kuacha Uanachama ........ 7
2.16 Mwanachama Sinzia ........ 8
2.17 Uteuzi wa Mrithi ........ 8
SEHEMU YA TATU ........ 9
3.0 AKIBA ........ 9
3.1 Utangulizi ........ 9
3.2 Aina ya Akiba ........ 9
3.3 Aina ya Mazao ya Akiba ya Hiari ........ 10
3.4 Uchangiaji wa Akiba ya Lazima ........ 10
3.5 Riba Juu ya Akiba ........ 10
3.6 Kukoma Uanachama ........ 10
3.7 Uhamasishaji Uchangiaji Akiba ........ 11
SEHEMU YA NNE ........ 11
4.0 AMANA

4.2 Aina ya Amana ........ 11
4.3 Taratibu za Uwekaji Amana ........ 12
4.4 Riba ya Amana Iliyofungwa ........ 12
4.5 Cheti cha Amana ya Muda Maalum ........ 12
4.6 Kuvunja Mkataba ........ 13
4.7 Kiwango cha Amana Iliyofungiwa ........ 13
SEHEMU YA TANO ........ 13
5.0 UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU ........ 13
SEHEMU YA SITA ........ 14
6.0 UWAZI JUU YA HUDUMA ZA MIKOPO ........ 14
6.1 Mikopo kwa Wanachama ........ 14
6.2 Uwazi katika Huduma za Mikopo ........ 14
6.3 Ufuatiliaji Madeni ........ 15
SEHEMU YA SABA ........ 15
7.0 MISINGI YA ULINZI WA MLAJI ........ 15
7.1 Mikutano Mikuu ........ 15
7.2 Mwonekano wa Maandishi katika Nyaraka za Chama ........ 16
7.3 Lugha ........ 16
7.4 Mabadiliko Mbalimbali ........ 16
7.5 Elimu ya Fedha ........ 16
8.0 SEHUMU YA NANE ........ 17
USHUGHULIKIAJI WA MALALAMIKO ........ 17
8.1 Njia za Kupokea Malalamiko ........ 17
8.2 Kamati za Kushughulikia Malalamiko ........ 17
8.3 Rejista ya Malalamiko ........ 18
8.4 Taarifa ya Malalamiko ........ 18
8.5 Utatuzi wa Migogoro ........ 18
SEHEMU YA TISA ........ 19
9.0 UHUISHAJI NA UIDHINISHAJI WA SERA ........ 19
9.1 Uhuishaji ........ 19
9.2 Uidhinishwaji wa Sera ........ 19

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Historia:

LESA SACCOS LTD ilianzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na.20 ya mwaka 2003.Kwa malengo ya kupokea akiba na kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa wamanachama wake. Mkutano mkuu wa wanachama ndicho chombo cha juu chenye mamlaka katika shughuli zote za chama na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinatambua kuwa bodi ya chama ndio chombo pekee cha kuongoza chama kwa kuzingatia ukasimishwaji wa madaraka hayo kupitia mkutano mkuu wa wanachama.

Kifungu Na.52 cha Sheria ya Vyama Vya Ushirika kinaenda mbali zaidi na kutoa nafasi kwa bodi kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia chama na miongoni mwa miongozo iliyotajwa ni pamoja na kanuni za uhasibu na fedha.

Dira ya chama ni kuondoa umaskini kwa kuhimiza uwekaji akiba mara kwa mara na kutoa mikopo pamoja na huduma zingine endelevu kiuchumi na kijamii kwa njia ya uzalishaji mali, utoaji wa huduma, biashara kilimo na ufugaji.

Mfungamano na Wanachama wa LESA SACCOS LTD ni watumishi wote wa Us Mission na watendaji wake.

### 1.2 Madhumuni ya kuwa na Sera hii:

Sera hii imetengenezwa ili kukidhi mahitaji ya Kifungu cha 50 ya Sheria Na. 10 ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 na Sehemu ya ix ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2019 ili kumlinda mlaji wa huduma

zinazotolewa na LESA SACCOS Ltd.

Hivyo, sera hii imegawanyika katika sehemu tisa zifuatazo; sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili juu ya taratibu za uwekaji wa hisa ndani ya Chama, sehemu ya tatu ni juu ya uchangiaji wa akiba, sehemu ya nne ni taratibu za uwekaji amana, sehemu ya tano ni taratibu utunzaji kumbukumbu, sehemu ya sita ni uwazi juu ya huduma za mikopo, sehemu ya saba ni misingi ya ulinzi wa mlaji, sehemu ya nane ni taratibu za kushughulikia malalamiko na sehemu ya tisa ni uhuishaji na uidhinishwaji wa Sera.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 HISA

**2.1** Maana ya Hisa**:**
Ni fungu linalotolewa na Mwanachama kama sehemu ya mtaji na umiliki wake kwenye Chama. Kifungu cha 41 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika na. 6 ya 2013 kinatambua Mwanachama (member) ni yule aliyenunua hisa ndani ya Chama na amelipia kwa angalau 50% na zaidi.

Hisa ni uwekezaji wa msingi kabisa kwa Mwanachama. Hisa itamwezesha Mwanachama kuwa mmiliki halali wa LESA SACCOS Ltd. Aidha, kila Mwanachama wa LESA SACCOS Ltd atatakiwa kuwa na kiwango cha chini cha Hisa (hisa za msingi) kisichopungua Tsh. 2,000,000/=

**2.2** Kiingilio**:**
Kiingilio kwa Mwanachama Mpya kitategemea kiwango kitakachoidhinishwa na Mkutano Mkuu. Kiingilio hakitarejeshwa endapo uanachama wa Mwanachama umekubaliwa na Bodi na Mkutano Mkuu. Kiingilio kwa sasa ni Tsh. 60,000/=.

## 2.3 Aina za Hisa:

Chama kina aina mbili za hisa ambazo Mwanachama anaweza kuchangia ambazo ni;

(i) Hiza za Msingi
(ii) Hisa za Hiari

Hisa za Msingi ndiyo hisa za umiliki wa Chama, ni kiwango cha chini cha hisa ambazo kila Mwanachama anatakiwa kumiliki tokea kujiunga Uanachama. Hadi sasa hisa za msingi kwa LESA SACCOS Ltd ni kama ifuatavyo:

- Kiwango cha chini cha idadi ya mafungu ya Hisa ni 200
- Thamani ya kila fungu la hisa ni TZS. 10,000/=
- Hivyo, kiwango cha chini cha thamani ya hisa kwa kila mwanachama ni TZS. 2,000,000/=

Kila mwaka Bodi ya uongozi itafanya tathmini juu ya kiwango cha hisa za msingi ili kujiridhilisha kama zinaendana na hali halisi ya uchumi ama zinaweza kuongezwa kwa kiwango kitakacho kubalika katika Mkutano Mkuu.

## 2.4 Hisa za Hiari:

Hisa za hiari ni kiwango chochote ambacho Mwanachama atachangia juu ya hisa za msingi. Hisa hizi huweza kuwekwa na Mwanachama muda wowote na pia zinaweza kupunguzwa muda wowote katika siku za kazi. Aidha, Bodi inaweza kuweka mpango maalum wa kungia mkataba maalum na Wanachama ili hisa za hiari ziwekezwe kwa muda maalum ndani ya Chama kwa ahadi ya kupatiwa faida ya riba itakayopangwa kulingana na hali halisi ya kifedha ndani ya Chama na uchumi wa nchi. Zao la hisa za hiari hutolewa na SACCOS yenye leseni daraja "B" kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

**2.5** Ulipaji wa Hisa

Mwanachama wa LESA SACCOS Ltd atatakiwa kuwa amelipia hisa angalau 100 zenye jumla ya thamani ya Shilingi 1,000,000 ndani ya kipindi kisichozidi miezi 12 tokea alipojiunga uanachama.

**2.6** Ukomo wa Hisa kwa Mwanachama

Hakuna Mwanachama wa LESA SACCOS Ltd ataruhusiwa kumiliki hisa zaidi ya 1/5 ya thamani ya hisa zote kwenye Chama.

**2.7** Kupunguza Hisa

Hisa za msingi haziwezi kupunguzwa wala kuchuliwa, katika tukio la Mwanachama kuacha, kuachishwa uanachama au kifo kiwango cha hisa anachomiliki kwenye Chama kitarejeshwa kupitia tengo la kukombolea mafungu; Endapo Chama kitakua hakina fedha ya kutosha katika tengo, Mwanachama atatakiwa kusubiri hadi pale hisa zake zitakapouzwa kwa Mwanachama mwingine.

Katika tukio la kifo cha Mwanachama, hisa zake zitarejeshwa kwa wasimamizi wa mirathi ama mrithi aliyeteuliwa kupitia fomu 8 ya Ushirika (iliyoko katika Jedwali la I la Kanuni za Vyama vya Ushirika, 2015)

**2.8** Taratibu za kupitishwa kuwa Mwanachama

Mwanachama mpya atajaza fomu ya maombi ya uanachama na kulipia kiingilio na hisa zake za msingi baada ya maombi yake kujadiliwa na bodi katika moja ya vikao vyake na maombi hayo yakipitishwa Mwanachama anaweza kuanza kupata huduma za Chama endapo amekaa kwa kipindi cha miezi 3 na ameshalipia angalau 50% na zaidi ya hisa alizoahidi kununua. Katika Mkutano Mkuu wa karibuni utakaofuata Bodi itawasilisha majina ya Wanachama wapya kwa ajili ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu huo.

## 2.9 Haki ya Kupatiwa Huduma

Kwa Mwanachama mpya atakua na haki ya uanachama kama vile kuhudhuria Mkutano Mkuu, kuomba nafasi ya uongozi na sifa ya kupatiwa huduma za Chama kama vile mikopo pale tu atakapokuwa amelipia angalau 50% ya hisa zake au zaidi.

## 2.10 Gawio

Hisa za msingi ni uwekezaji ambao unamwezesha Mwanachama kupata gawio baada ya hesabu za Chama kukaguliwa, kodi kulipwa na matengo ya kisheria kutengwa. Lakini pia gawio litalipwa endapo Chama kina kiwango cha mtaji unaokidhi yaani; uwiano kati ya mtaji tete na mali uwe 8% au zaidi, uwiano kati ya mtaji taasisi/msingi na mali uwe 6% au zaid na uwiano wa hisa zilizolipwa kikamilifu na mali uwe 2% au.

Mkutano Mkuu ndiyo wenye mamlaka ya kupitisha kiwango cha gawio na mfumo wa ulipaji gawio hilo baada ya Chama kukidhi mtaji unaotakiwa.

Endapo Chama kitakuwa kimekidhi vigezo vya mtaji unaotakiwa kisheria, taratibu zifuatazo zinaweza kufuatwa kwenye ziada halisi kwa ajili ya gawio:

(i) Kiasi cha asilimia ya ziada halisi kwa ajili ya honoraria kwa viongozi.

(ii) Kiasi cha asilimia ya ziada halisi kwa ajili ya bonasi kwa Watendaji waliofikia malengo kwa mujibu wa taratibu zilizoweka katika Sera ya Utumishi

(iii) Kiasi cha asilimia ya ziada halisi kwa ajili ya motisha kwa Wanachama waliowekeza akiba zao kwa wingi na Wanachama

waliochangia mapato zaidi kwenye Chama ndani ya mwaka wa fedha husika kwa uwiano na jinsia.

(iv) Kiasi cha asilimia ya ziada halisi kama limbikizo la ziada.

(v) Mapendekezo juu ya kiwango cha fedha kilichobaki, yaani 75% kutoka kwenye ziada halisi kitatolewa kama gawio kwa Wanachama waliolipia hisa zao za msingi kwa 50% na zaidi. **Gawio sharti litolewe kwenye hisa za msingi tu.** Kwa kuzingatia kwamba gawio ni kwa ajili ya mwaka wa fedha husika na ili kuwa na usawa, gawiwo litalipwa kwa Mwanachama kulingana na muda ambao hisa zake zimekaa Chamani ndani ya mwaka (miezi 12). Hivyo, kanuni ifuatayo itatumika kufikia kiasi cha gawiwo stahili kwa kila Mwanachama.

**Thamani ya gawio kwa kila hisa =** <u>Fedha zote kwa ajili ya</u>
**gawio** Jumla ya Idadi ya
Hisa

**Kiasi cha Gawio kwa kila Mwanachama = (A x B) x C/12**

**A** = Idadi ya Hisa za Msingi anazomiliki Mwanachama
**B** = Thamani ya gawio kwa kila hisa
**C** = Muda (miezi) ambao hisa za Mwanachama zimekaa Chamani ndani ya mwaka wa fedha husika

(vi) Utekelezaji wa mapendekezo haya na maazimio ya Mkutano Mkuu lazima yapate idhini ya Mrajis kabla ya mgawanyo wa ziada halisi ikiwemo gawio kulipwa.

Chama hakitatoa gawio kwa fedha taslimu bali fedha ya gawio

italipwa kwenye akaunti ya Amana ya Mwanachama.

***NB:*** Bodi kwa kushauriana na Ofisi ya Mrajis inaweza kuwashauri Wanachama gawio litolewe kwa njia ya kuongeza thamani kwenye hisa za kila Mwanachama badala ya kuchukuliwa.

### 2.11 Uhamishaji wa Hisa

Hisa za msingi haziwezi kuhamishika, Mwanachama anaruhusiwa kuhamisha hisa zake za hiari kwenda kwenye akiba zake kama atataka kujazia akiba kwa ajili ya kuongeza uwiano wake wa akiba na mkopo.

### 2.12 Hisa Kutumika Kama Dhamana ya Mkopo

Mwanachama anaweza kutumia hisa zake za hiari kama dhamana ya mkopo isipokuwa **Hisa za msingi HAZIWEZI** kutumika kama dhamana ya mkopo.

### 2.13 Cheti cha Hisa

Kila mwanachama anayemaliza kulipia hisa zake zote za msingi atapewa cheti cha hisa kuthibitisha umiliki wake kwenye SACCOS. Cheti cha hisa kinaweza kubadilishwa kutokana na ongezeko la thamani za hisa alizonazo Mwanachama au mabadiliko yoyote yanayoweza kujitokeza kwa kuhuisha Masharti ya Chama.

### 2.14 Hisa Kushirikiliwa kama Mali katika mchakato wa Ufilisi

Kifungu cha 63 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika na. 6 ya mwaka 2013 kinakataza hisa za Mwanachama na mawekezo yake mengine kushikiliwa (attachment) kama mali za mdaiwa wakati wa mchakato wa ufilisi (endapo Mwanachama ndiyo mfilisiwa).

### 2.15 Kuacha Uanachama

Endapo mwanachama ataacha uanachama kwa sababu yoyote ile

Chama hakitarudisha hisa za msingi kupitia kasma ya hisa za Chama isipokuwa Chama kitamrejeshea hisa zake kupitia fedha zilizoko katika tengo la kukombolea hisa.

Endapo Chama hakina fedha za kutosha kwenye kasma ya tengo la kukombolea hisa, Mwanachama ataruhusiwa kuuza hisa hizo kwa Mwanachama mwingine au kama Chama kitakua katika hali nzuri ya ukwasi basi kitanunua hisa hizo ili kumpatia fedha mwanachama aliyeacha uanachama na kuziuza kwa mwanachama mwingne mpya au anayeendelea.

## 2.16 Mwanachama Sinzia

Chama kitachukulia Mwanachama sinzia endapo hakuna muamala wowote umefanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, pia Chama kitachukulia akaunti kuwa imeachwa baada ya miaka 5 bila kupokea mawasiliano yoyote kimaandishi kutoka kwa mwanachama mwenyewe au mrithi wake. Na fedha katika kasmi hii zitatolewa na kuwekwa kwenye kasma maalum ya tengo la Hisa zilizoachwa kwa muda wote.

Endapo Mwanachama atajitokeza basi fedha hizo zitarejeshwa kwenye akuanti ya kawaida kama atahitaji kuendelea na uanachama na kama la basi atarejeshewa stahiki zake. Endapo mrithi wa mwanachama ndio atakayejitokeza basi stahiki za Mwanachama husika zitakabidhiwa kwa mrithi huyo baada ya kujiridhisha uhalali wake kwa mujibu wa taratibu na mirathi.

## 2.17 Uteuzi wa Mrithi

Kuchagua au kubadilisha mrithi ni moja ya haki ya msingi kwa kila Mwanachama. Na kwa mujibu wa Kanuni ya 37 ya Vyama vya Ushirika, 2015 kila Mwanachama lazima awasilishe kwenye Chama jina au majina ya Mrithi wake kwa kujaza fomu nambari 8 iliyopo katika jedwali la kwanza la Kanuni hii.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 AKIBA

### 3.1 Utangulizi

Akiba ni fedha anazochangia Mwanachama ili kuwa na sifa ya kupata huduma za mikopo. Fedha hii hairuhusiwi kutoka ama kupungua mara kwa mara isipokuwa kama ilivyoelekezwa katika Masharti ya Chama.

### 3.2 Aina ya Akiba

Kutakuwa na makundi makuu mawili ya Akiba

(i) Akiba ya lazima.

(ii) Akiba ya hiari.

**Akiba ya lazima**

Akiba ya lazima inamfanya Mwanachama kuwa na sifa ya kupata huduma ya mikopo na akiba hii inaweza kupunguzwa ama kama inavyoelekezwa kwenye Masharti ya Chama. Kwa mujibu wa Sera hii, Mwanachama atatakiwa kuchangia akiba zake kila baada ya wiki mbili kwa kiwango kisichopungua Tsh. 60,000/= pia Mwanachama anaruhusiwa kuchangia zaidi ya kiwango cha chini kutokana na uwezo wake.

**Akiba ya Hiari**

Akiba ya hiari ni akiba anayojiwekea Mwanachama kwa malengo maalum, akiba hii inaweza kutolewa ama kupunguzwa muda wowote.

### 3.3 Aina ya Mazao ya Akiba ya Hiari

Chama kitakapokuwa kimekamilisha miundombinu ya upokeaji akiba mbalimbali za hiari Mwanachama anaweza kuweka akiba yake ya hiyari katika moja ya mazao yafuatayo:-

- Akiba ya Malengo Maalum
- Akiba ya Watoto
- Akiba ya Elimu
- Akiba ya Sikukuu
- Mfuko wa Jamii
- Akiba ya Majanga
- Akiba ya Biashara

### 3.4 Uchangiaji wa Akiba ya Lazima

Kila Mwanachama atatakiwa kuchangia kiwango cha chini cha akiba kwa Tsh. 60,000/= Kila baada ya wiki mbili. Mwanachama anaruhusiwa kuwekeza akiba zaidi ya kiwango cha chini kilichowekwa, "*Wekeza akiba ni mali yako*", itakufaa sana siku za usoni kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha.

### 3.5 Riba Juu ya Akiba

Kupitia Mkutano Mkuu Kutakuwa na maamuzi ya kuweka kiwango cha riba juu ya akiba za Wanachama ili kuwezesha ongezeko la thamani ya akiba hizo. Kwa kuwa hii ni gharama ya kifedha kwa Chama itakuwa inabadilika kila mwaka pale itakapobidi kwa makubaliano ya Wanachama kutokana na mwelekeo wa makisio ya mapato na matumizi na hali halisi ya uchumi wa nchi .

### 3.6 Kukoma Uanachama

Mwanachama akikoma kuwa Mwanachama wa LESA SACCOS Ltd atatakiwa kumwandikia barua Mwenyekiti wa Bodi kuonesha kusudio lake la kujiondoa uanachama, na endapo ombi likiridhiwa akiba za Mwanachama na stahili nyinginezo zitarejeshewa ndani ya

siku 60 tokea kupokelewa na notisi ya kusudio la kujitoa uanachama.

Endapo Mwanachama ana mkopo ama amedhamini mkopo hatarejeshewa stahili zake hadi pale mkopo wake ama udhamini wake utakapolipwa kikamilifu.

### 3.7 Uhamasishaji Uchangiaji Akiba

Bodi ya Chama itakuwa na programu mbalimbali za kuhamasisha ongezeko la akiba kutoka kwa Wanachama wake kama vile kuendesha michezo ya bahati nasibu, promosheni, uzengezi, kutoa huduma ambatishi (embedded products) na mbinu nyinginezo kama zitakavyoelekezwa katika Mpango Biashara wa Chama.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 AMANA

### 4.1 Utangulizi

Amana ni kiwango chochote cha fedha anayoiweka mwanachama kwa lengo la kujiwekea akiba inayoweza kumsaidia badae. Amana ni fedha inayoweza kuwekwa muda wowote na kutolewa ama kupunguzwa kwa muda wowote.

### 4.2 Aina ya Amana

Ili kuendesha Chama kibiashara, Bodi ya LESA SACCOS Ltd inaweza kuongeza zao lingine la amana ili kuwawezesha Wanachama kuweka na kuchukua fedha kwa urahisi katika Chama chao. Kwa mukutadha wa Sera hii, na endapo Bodi itaona iko tayari kupokea amana, yafuatayo ni makundi 2 makuu ya aina za amana ambayo

zitatolewa; -

(i) Amana ya Wazi
(ii) Amana Iliyofungwa

Amana ya wazi ni fedha anayoiwekwa au kutolewa na Mwanachama muda wowote.

Kwa upande mwingine **amana iliyofungwa** ni amana ambayo Mwanachama anaingia makubaliano au mkataba na Chama kutoichukua amana yake kwa muda uliokubaliwa kwa ahadi ya Chama kumlipa riba ndani ya kipindi cha makubaliano. Viwango vya riba katika amana iliyofungwa vitatokana na hali ya biashara pamoja na viwango vya soko la fedha.

## 4.3 Taratibu za Uwekaji Amana

Chama kitaanzisha fomu maalum kwa ajili ya Mwanachama kujaza na kuweka amana. Amana hiyo ikipokelewa itaingizwa kwenye leja kadi ya mwanachama husika na stakabadhi kutolewa.

## 4.4 Riba ya Amana Iliyofungwa

LESA SACCOS Ltd itaweka viwango vya riba juu ya amana iliyofungiwa na maboresho yake yanaweza kufanyika kila mwaka kutokana na makisio ya mapato na matumizi na hali ya uchumi.

Kwa sasa inapendekezwa riba juu ya amana ni 9.5% kwa mwaka na riba husika hulipwa katika vipindi vya kila robo mwaka.

## 4.5 Cheti cha Amana ya Muda Maalum

Mwanachama aliyeweka amana iliyofungwa atapewa cheti **(certificate of deposit)** cheti hicho kitakuwa na tarehe ya kuweka na kuiva, jina la mwanachama, kiwango cha fedha zilizoweka, riba, muda na sahihi mbili ya Mwenyekiti na Meneja wa SACCOS.

**4.6** Kuvunja Mkataba

Endapo mwanachama atavunja mkataba kwa kuhitaji fedha zilizo kwenye amana iliyofungiwa kabla ya muda wa kuiva kufika atalipia fidia kwa kugawana na Chama faida iliyopatikana kwa uwiano wa 50% kwa 50%. Na kama amana hiyo itakuwa haijazaa faida yoyote Mwanachama atalipia fidia ya usumbufu ya kiasi cha Tsh. 10,000/=.

**4.7 Kiwango cha Amana Iliyofungiwa**

Kiwango chochote cha fedha ya amana ndani ya Chama kiweza kupata riba inayolipwa kila robo mwaka.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Ofisi ya Chama itahakikisha inaandika na kutunza kumbukumbu zote zinazohusiana na hisa, akiba na amana za kila mwanachama kwa wakati, usahihi na usalama.

Mwanachama, kwa upande wake, atahakikisha kuwa: -

i. Anapewa stakabadhi ya malipo ya hisa, akiba na amana aliyofanya kupitia aina yoyote ya makusanyo (makato ya moja kwa moja kwenye mshahara, taslimu ama kuweka benki).
ii. Leja kadi (Kitabu) ya Mwanachama itajazwa kwa usahihi kulingana na hisa, akiba na amana alizolipa.
iii. Anatunza kumbukumbu zote zinazohusiana na malipo au punguzo la akiba ama amana zake.
iv. Anatunza hati za mishahara zote zinazohusiana na makato ya akiba.
v. Anakuwa huru kuhakiki ushahihi wa hesabu yake ya hisa, akiba na amana kwa kufika ofisini na kufanya malinganisho (reconciliation) kati ya hesabu zake na hesabu zilizotunzwa ofisini.

Aidha, Chama kitaendelea kuwekeza na kuboresha matumizi ya mifumo ya

TEHAMA ili kutunza kumbukumbu kwa kutumia mifumo hiyo na kuboresha utoaji huduma kwa Wanachama. Mifumo hii itarahisisha uwekaji hisa, akiba na amana lakini pia mwanachama anaweza kupata taarifa zake za Chama kwa haraka na usahihi.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 UWAZI JUU YA HUDUMA ZA MIKOPO

### 6.1 Mikopo kwa Wanachama

Wanachama wote wa LESA SACCOS Ltd wana haki sawa ya kupatiwa huduma za mikopo. Tofauti katika huduma za mikopo inaweza kujitokeza kulingana na mahitaji ya Sheria, Kanuni, Masharti ya Chama na Sera ya Mikopo. Tofauti hizi zinakubaliwa na Wanachama wote katika Mkutano Mkuu; tofauti ni kama vile uwezo wa kurejesha, malengo ya mkopo, aina ya mkopo, n.k.

### 6.2 Uwazi katika Huduma za Mikopo

Utoaji wa mikopo utakwenda sambamba na uwazi wa upangaji bei pamoja na utengenezaji na uidhinishwaji wa sera na taratibu za mikopo kupitia Mikutano Mikuu ya Wanachama. Kwa mujibu wa Kanuni ya 36 ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2019, Bodi inaweza kupanga bei, gharama na adhabu za ucheleweshaji wa mikopo na kabla ya kuanza kutumika kwa bei mpya, sharti Wanachama wajulishwe kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo kubandika notisi ya kuongeza bei na gharama za mikopo kwenye mbao za matangazo, barua pepe na ujumbe mfupi wa maneno.

Notisi ya kuongeza bei na gharama za mkopo itakuwa si chini ya miezi mitatu. Bei na gharama za mikopo endapo zitapanda, zitahusika na mikopo mipya itakayotolewa baada ya tangazo.

### 6.3 Ufuatiliaji Madeni

Kama taratibu zilivyowekwa katika Sera ya Ufuatiliaji madeni, Mwanachama atapewa muda wa kutosha kujieleza lakini pia kutoa mpango mbadala wa kulipa deni lake. Endapo hatua zote za kumpa muda zikishindikana, taratibu za kisheria zitafuata kwa kumuandikia notisi (demand notice) za siku 21 mara 3; hivyo jumla ya siku za notisi ni 63 baada ya hapo atapewa tena barua ya kisheria ya siku 30 ili Chama kianze kutumia ama kuuza dhamana zake kulipia mkopo.

Zoezi la ufuatiliaji madeni litazingatia haki za binadamu za kujali utu na heshima. Endapo Chama kitatumia Madalali wa kukusanya madeni, kutakua na mkataba maalum wa kuzingatia haki za mteja katika zoezi la ukusanyaji madeni ikiwemo muda maalum wa kufanya mawasiliano na Mwanachama, maeneo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa kumfuata Mwanachama, kupata ridhaa ya Mwanachama kabla ya kumtaarifu Mwajiri wake mpya.

Aidha, Mdhamini wa mkopo naye pia atapewa nakala ya taarifa inayokwenda kwa mkopaji katika kila hatua ya ufuatiliaji madeni.

## SEHEMU YA SABA

## 7.0 MISINGI YA ULINZI WA MLAJI

### 7.1 Mikutano Mikuu

LESA SACCOS Ltd itahakikisha angalau Mkutano Mkuu mmoja kwa mwaka ili Wanachama wapate taarifa mbalimbali, mipango na kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na uendeshaji wa shughuli za Chama.

Kila kitu kinachofanyika kwenye Chama kinakua kimeazimiwa na Mkutano Mkuu.

### 7.2 Mwonekano wa Maandishi katika Nyaraka za Chama

LESA SACCOS Ltd itahakikisha maandishi katika nyaraka mbalimbali za Chama yanaonekana na kusomeka kwa hati nzuri. Nyaraka za Chama zinazohusika hapa ni pamoja na fomu mbalimbali, mikataba, barua na makablasha ya Mkutano Mkuu.

### 7.3 Lugha

Katika mawasiliano kwa njia mbalimbali, LESA SACCOS Ltd itatumia lugha inayoeleweka kwa Wanachama wengi. Inapolazimika, tafsiri ya lugha itafanyika ili kuhakikisha Lugha ya Kiswahili inatumika katika nyaraka, mawasiliano na makubaliano yote ya Chama.

### 7.4 Mabadiliko Mbalimbali

Katika uendeshaji wa shughuli za Chama kunaweza kutokea mabadiliko mbalimbali yanayohitaji kujulikana kwa Wanachama. Bodi ya Chama itapima kiwango, aina na athari za mabadiliko na maamuzi yanaweza kuwa kuitisha Mkutano Mkuu Maalum ili kuwahabarisha Wanachama ama kutoa taarifa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile mbao za matangazo, barua pepe, ujumbe mfupi wa simu (SMS), n.k.

Ni lazima mabadiliko yoyote ndani ya Chama yatangazwe kwa Wanachama na yale ambayo Bodi itaona yanahitaji maamuzi ya Wanachama, itaitishwa Mkutano Mkuu Maalum.

### 7.5 Elimu ya Fedha

Wanachama wa LESA SACCOS Ltd wana kofia mbili (2) ndani ya Chama yaani ni Wamiliki wa Chama na wakati huo huo ni Wateja wa huduma zinazotolewa na Chama. Hivyo, Chama kitahakikisha kinatoa elimu ya fedha kwa Wanachama kwa kutumia njia na mbinu mbalimbali kama vile semina, vipeperushi, kuwashirikisha baadhi ya Wanachama katika baadhi ya shughuli za Bodi, matangazo kwenye mbao, tovuti ya Chama pamoja na kuwa na mitandao ya kijamii inayofanya kazi (interactive). Katika makisio

ya mapato na matumizi ya kila mwaka, LESA SACCOS Ltd itaweka bajeti maalum kwa ajili ya elimu ya fedha kwa Wanachama wake.

## SEHUMU YA NANE

## 8.0 USHUGHULIKIAJI WA MALALAMIKO

### 8.1 Njia za Kupokea Malalamiko

Chama kitaweka miundombinu stahiki ya kupokea mrejesho na malalaimiko ya Wanachama. Njia hizo ni pamoja na kuwa na sanduku la maoni litalowekwa katika sehemu ya wazi na funguo zake zitatunzwa na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi, mitandao ya kijamii kama vile "facebook", "instagram" na "Twitter", barua pepe ya Chama, tovuti ya Chama pia itakuwa na chumba cha kutoa malalamiko pamoja na njia nyingine ambazo Bodi itaona zinafaa.

### 8.2 Kamati za Kushughulikia Malalamiko

#### 8.2.1 Kamati ya Usimamizi

Kamati ya Usimamizi ina jukumu la kupokea malalamiko ya Wanachama na kuyawasilisha kwenye Bodi kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Hivyo, Wanachama wataelekezwa endapo wana malalamiko yayohusiana na shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Chama, wayawasilishe kwa Kamati ya Usimamizi.

#### 8.2.2 Bodi

Mwenyekiti wa Bodi atapokea malalamiko juu ya Mikopo na kuyawasilisha kwenye Bodi nzima kwa ajili ya maamuzi. Hivyo, Wanachama wanatakiwa kupelekea malalamiko juu ya mikopo moja kwa moja kwa Mwenyekiti wa Chama kimaandishi. Aidha, Bodi itapokea malalamiko yaliyopokelewa na Kamati ya Usimamizi na kuyafanyia kazi.

#### 8.2.3 Meneja

Meneja wa Chama kama mtendaji mkuu anaweza kuunda kamati ya

kushughulikia malalamiko ya Wanachama kwa kiwango cha yale yanayokuja moja kwa moja kwenye Chama. Pia Meneja anaweza kuteua Mtendaji mmoja wapo ili pamoja na majukumu yake ya msingi, ashughulikie pia suala la malalamiko ya Wanachama kwa kuyapokea, kuyawasilisha sehemu husika, kufuatilia hali ya utekelezaji na kutoa mrejesho kwa Mwanachama kwa wakati.

### 8.3 Rejista ya Malalamiko

Chama kitakua na rejista ya malalamiko kwa ajili ya kusajili kila aina ya malalamiko yanayokuja kwenye Chama. Pia rejista itakuwa na sehemu ya kujaza tarehe ya kupokelewa na hali halisi ya utekelezaji kwa kila lalamiko. Pamoja na kusajili malalamiko, rejista itatumika kama rejea katika ufuatiliaji na pia kusaidia Chama kuelewa maeneo ya uendeshaji yanayolalamikiwa sana na kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

### 8.4 Taarifa ya Malalamiko

Meneja atapokea taarifa fupi ya hali ya malalamiko kila siku kabla ya kufunga ofisi; pia, Kila mwezi Mtendaji anayehusika na kupokea malalamiko ya Wanachama ataandaa taarifa ya malalamiko na kuiwasilisha kwenye Menejimenti.Kila robo mwaka, Meneja ataanda taarifa ya malalamiko na kuiwasilisha kwenye Bodi.

### 8.5 Utatuzi wa Migogoro

Malalamiko yasipopatiwa ufumbuzi kwa wakati yanaweza kubadilika na kuwa migogoro ama Mwanachama asipokubaliana na majibu au namna malalamiko yake yanavyoshughulikiwa inaweza kutokea hali ya migogoro.

Migogoro ndani ya Chama itatatuliwa kwa njia ya amani na mazungumzo. Migogoro yote lazima iingizwe kwenye rejista na itashughulikiwa ndani ya siku 15 tokea kupokelewa kwake.

Endapo, Mwanachama hataridhika na maamuzi yaliyofanywa na Chama

kupitia Bodi, anaweza kukata rufaa kwa Mrajis Msaidizi wa Mkoa ndani ya siku 30 tokea maamuzi wa Bodi yatoke ama utatuzi ufanyike. Endapo Mwanachama atakuwa hajaridhika na maamuzi ya Mrajis Msaidizi wa Mkoa, anaweza kukata rufaa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Taifa, endapo pia kama Mwanachama hataridhika na maamuzi ya Mraji Taifa, atakata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana na usimamizi ya Ushirika; maamuzi ya Waziri yatakuwa na mwisho.

## SEHEMU YA TISA
## 9.0 UHUISHAJI NA UIDHINISHAJI WA SERA

### 9.1 Uhuishaji
Sera hii itahuishwa mara mara kutokana na mahitaji na hali ya soko la sekta ya fedha

### 9.2 Uidhinishwaji wa Sera
Sera hii imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya LESA SACCOS LTD kwa niaba ya wanachama kwa kibali cha Mrajis katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Julai 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika

..........................
......................
**Mwenyekiti**

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
23 NOV 2020
KINONDONI
DAR-ES-SALAAM

**Meneja**

TANZANIA
Approved this 20TH
day of JANUARY 2021
..........................
Asst. Registrar of Cooperative Societies